SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA

MHE. KHAMIS JUMA MWALIM (MBM)

KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI

KUHUSU MAKADIRIO YA

MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA

WA FEDHA 2020/2021

MEI, 2020

YALIYOMO

UTANGULIZI 1
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA 2010/2020..... 5
MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 11
Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo kwa Mwaka 2019/2020 . 12
G10 – Wizara ya Katiba na Sheria 12
G02 – Mahakama 23
G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu..... 28
G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka 32
G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria 33
MUELEKEO WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 35
Vipaumbele vya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2020/2021..... 35
G10 – Wizara ya Katiba na Sheria..... 37
G02 – Mahakama 42
G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali..... 43
G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka 43
G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria 45
SHUKURANI 45
HITIMISHO..... 48
Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2019/20..... 50
Kiambatanisho 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021..... 54

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2019/2020 na Makadirio ya 2020/2021 60
Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2020/2021 61
Kiambatanisho 5a: Muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria .. 63
Kiambatanisho 5b: G10 – Programu Kuu, Programu Ndogo na Huduma 64
Kiambatanisho 6a: Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2019/2020 66
Kiambatanisho 6b: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Mwanzo 2019/2020 69
Kiambatanisho 6c: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Kadhi 2019/2020 70
Kiambatanisho 7a: Miswada ya Sheria 2019/20 71
Kiambatanisho 7b: Matangazo ya Kisheria - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu 2019/20 73
Kiambatanisho 8a: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji 2019 – UTAHIZA 77
Kiambatanisho 8b: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji - BAKWATA 79

HOTUBA YA WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA

MHE. KHAMIS JUMA MWALIM (MBM)
KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** naomba kutoa hoja kwamba Baraza lako tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili liweze kupokea, kujadili na kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

2. **Mheshimiwa Spika,** kabla sijaendelea na hotuba yangu, naomba nichukue fursa hii kutoa salamu za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kufuatia kifo cha aliyekuwa Waziri wa Katiba na Sheria wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Balozi Dkt. Augustine Philip Mahiga. Aidha, natoa salamu za rambirambi kufuatia kifo cha aliyekuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Mheshimiwa Augustino Stephen Lawrence Ramadhani.

3. **Mheshimiwa Spika,** natoa salaam za rambirambi kwa Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Ali Mohamed Shein, kufuatia kifo cha aliyekuwa Jaji Mkuu wa Zanzibar Mhe. Ali Haji Pandu. Aidha, natoa salamu za rambirambi kufuatia kifo cha aliyekuwa Kadhi Mkuu wa Zanzibar, Sheikh Habibu Ali

Kombo. Vile vile, natoa salamu za rambirambi kufuatia kifo cha aliyekuwa Jaji wa Mahakama Kuu Mheshimiwa. Mkusa Isaack Sepetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awape subira wote walioguswa na misiba hii.

4. **Mheshimiwa Spika,** awali ya yote, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema, kwa kutujaalia kukutana ili kujadili utekelezaji wa majukumu yetu kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 na kueka mwelekeo wa mwaka wa fedha 2020/2021.

5. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kumshukuru Mwenyezi Mungu, natoa pongezi zangu za dhati kwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kuendelea kuliongoza vyema Taifa letu. Aidha, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa hatua zake anazochukua za kuilinda jamii ya Wazanzibari katika kupambana na ugonjwa ulioingia wa virusi vya korona ambao unaitikisa Dunia. Tunamwomba Mwenyezi Mungu atuondolee mtihani huu na awaponeshe kwa haraka wale wote waliopata ugonjwa huu, amin.

6. **Mheshimiwa Spika,** naomba niendelee kumpongeza Dkt. Ali Mohamed Shein, katika kutekeleza kwa kiwango kikubwa Ilani ya CCM ya 2015-2020. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amwongoze vyema Rais wetu katika kuelekea kwenye Uchaguzi Mkuu.

7. **Mheshimiwa Spika,** pongezi zangu za dhati zimwendee Msaidizi Mkuu wa Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Mwakilishi wa Jimbo la Mahonda kwa kutekeleza vyema majukumu yake. Hakika uwezo wake wa kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali umeacha alama inayofaa kuigwa. Kwa ujumla tunawashukuru viongozi wetu hawa na kuwaombea kwa Mwenyezi Mungu awape afya njema wao na familia zao.

8. **Mheshimiwa Spika,** naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Machano Othman Said, Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ambaye ni Mwakilishi wa Wananchi wa Jimbo la Mfenesini, Makamu wake Mheshimiwa Zulfa Mmaka Omar Mwakilishi wa Viti Maalum wa Vijana Mkoa wa Kusini Pemba na Wajumbe wote wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora na Idara Maalum ya Baraza la Wawakilishi kwa mwongozo wao walioipatia Wizara ya Katiba na Sheria katika kipindi chote cha uongozi wao.

9. **Mheshimiwa Spika,** nampongeza pia Mheshimiwa Rashid Makame Shamsi, Mwenyekiti wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo na Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Magomeni, Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma Mwakilishi wa Wananchi Jimbo la Chukwani pamoja na Wajumbe wote wa Kamati hiyo. Hakika katika kipindi kifupi cha kufanyakazi kwa kamati hii, tumeweza kufanya kazi nzuri inayopaswa kuendelezwa

katika kipindi kijacho. Nitakuwa mkosefu wa fadhila bila ya kuwapongeza Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wote wa Kamati za Baraza lako Tukufu kwa kushirikiana nasi kutekeleza majukumu yetu. Changamoto zilizokuwa zinaibuliwa na Waheshimiwa Wawakilishi zimechangia kwa kiasi kikubwa kuleta maendeleo katika taifa letu.

10. **Mheshimiwa Spika,** naomba kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Baraza la Wawakilishi, pamoja na Kamati ya Uongozi ya Baraza la Wawakilishi kwa kuliongoza vyema Baraza letu tukufu. Nachukua fursa hii pia kumpongeza Katibu wa Baraza la Wawakilishi kwa utendaji wake mzuri. Watendaji wote wa Baraza lako tukufu nao ninawapongeza kwa ushirikiano mzuri waliotupatia wakati wa shughuli za Baraza.

11. **Mheshimiwa Spika,** mwisho lakini si kwa umuhimu, naishukuru familia yangu kwa kunipatia utulivu na msaada ulioniwezesha kutekeleza majukumu yangu kwa ufanisi. Shukurani za dhati ziwaendee wananchi wa Jimbo la Pangawe kwa kuniunga mkono na kufanyakazi pamoja nami kwa kipindi chote cha 2015/2020. Ni matumaini yangu kuwa hawataniacha mkono ili yale mazuri tuliyoyaanza tuweze kuyaendeleza katika kipindi kijacho.

12. **Mheshimiwa Spika,** hotuba hii itahusisha Utangulizi ambao tayari nimeshauwasilisha, Mapitio ya Utekelezaji wa Ilani kwa Kipindi cha 2010 - 2020, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Malengo kwa mwaka wa fedha 2019/2020,

Muelekeo wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Shukrani na hatimaye Hitimisho.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA ILANI YA CHAMA CHA MAPINDUZI KWA KIPINDI CHA 2010/2020

13. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria imetekeleza vyema Ilani ya Uchanguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa kipindi kilichotajwa hapo juu kama ifuatavyo:-

14. **Mheshimiwa Spika,** Mfumo wa Sheria umeimarika kutokana na kuzifanyia mapitio sheria, kanuni na mikataba inayozingatia mahitaji ya wakati uliopo. Sheria ya Mahakama ya Biashara namba 9/2013, Sheria ya Mahakama ya Kadhi namba 9/2017, Sheria ya Ushahidi namba 9/2016, Sheria ya Adhabu namba 6/2018, na Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 7/2018 zimefanyiwa mapitio yaliyopelekea kuondoa upungufu uliokuwepo. Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu namba 6/2013, Sheria ya Usimamizi wa Mahakama namba 11/2018, Sheria ya Msaada wa Kisheria namba 13/2018, Sheria ya Skuli ya Sheria namba 13/2019, na Sheria ya Mawakili zimetayarishwa na baadhi yao kuanza kutumika. Zana hizi za kufanyia kazi pamoja na mabadiliko ya kimaendeleo katika Taasisi za Sheria Zanzibar zimepelekea sekta ya sheria na upatikanaji wa haki kuimarika.

15. **Mheshimiwa Spika,** sheria nyingine ambazo zina msukumo mkubwa katika maisha ya wananchi zimetungwa ikiwemo

Sheria ya Usajili wa Biashara na Mali namba 13/2012, Sheria ya Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii namba 3/2018 (Civil Status Registration Agency Act 3/2018), Sheria ya Kamisheni ya Ardhi namba 6/2015 zimetungwa. Utendaji kazi wa Mahakama ya Kazi kupitia Kitengo cha Usuluhishi wa Migogoro ya Kazi (Labour Dispute Handling Unit) umeimarika na kusaidia kupunguza mrundikano wa kesi zinazohusiana na masuala ya kazi, umeongeza ushirikiano baina ya mahakama na wahusika wa mahakama hiyo na pia kupunguza mizozo baina ya Waajiri na Waajiriwa. Aidha, utendaji kazi wa Mahakama hiyo umeimarisha utekelezaji wa uamuzi unaotolewa na mahakama kuhusu ulipaji wa fidia au kurudishwa kazini.

16. **Mheshimiwa Spika,** mbali na kuimarika kwa taasisi kongwe za sheria, hatua za karibuni za kuanzisha Skuli ya Sheria Zanzibar zitasaidia kuimarisha zaidi wanasheria wetu na kuwaweka katika viwango vinavyokubalika kitaifa na kimataifa. Napenda kuchukua fursa hii kulijulisha Baraza lako tukufu kuwa maandalizi ya uanzishwaji wa Skuli ya Sheria yanaendelea vyema. Uchambuzi wa mahitaji ya bajeti umefanyika na kuanzia mwaka 2020/2021, Skuli ya Sheria imetengewa ruzuku ya kuiendesha.

17. **Mheshimiwa Spika,** kufanyakazi kwa mfumo wa msaada wa kisheria hapa Zanzibar, kulikopelekea, pamoja na mambo mengine, kuweka misingi bora zaidi ya utendajikazi wa Mawakili na kutambulika rasmi kwa Wasaidizi wa Sheria ni katika masuala ya kujivunia. Hivi leo

watoa huduma za msaada wa kisheria walioenea sehemu zote Unguja na Pemba wamekuwa msaada mkubwa kwa wananchi wanaokabiliwa na changamoto mbali mbali. Aidha, Sheria ya Mawakili na ile ya Jumuiya ya Mawakili zimeweka misingi ya ufanyajikazi kwa kuzingatia umahiri na maadili ya kisheria. Kituo cha Mafunzo na Utafiti wa Sheria kimeendelea kutoa taaluma kwa watu mbali mbali na kuwawezesha kunyanyua viwango vyao vya ufahamu wa sheria katika utendaji wao.

18. **Mheshimiwa Spika,** uimarishaji wa Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali umeiwezesha Ofisi hiyo kufanyakazi zake kwa ufanisi. Aidha, Usimamizi wa Mikataba umeimarika ambapo jumla ya rasimu za mikataba 1,394 na MoU 235 zinazohusiana na masuala ya elimu, afya na kilimo zilipitiwa na kutolewa ushauri. Vile vile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa miswada ya sheria 112, ambapo baadhi ya sheria hizo zilikuwa zimepitwa na wakati na zilikuwa kikwazo katika upatikanaji wa haki. Ofisi pia iliweza kutengeneza kanuni 181 na matangazo ya kisheria 1,303.

19. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ina jukumu la kusimamia kesi za madai iwapo Serikali itashtaki au itashtakiwa. Kwa kipindi cha Januari 2011 hadi Machi 2020 jumla ya kesi 142 zilisimamiwa kati ya hizo kesi nane zilimaliza kwa makubaliano nje ya mahakama, kesi 112 zimemalizika ambapo kesi 67 Serikali imeshinda na kesi 12 imeshindwa. Jumla ya kesi 22 bado zinaendelea kusimamiwa.

20. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imeendelea kusimamia utaratibu wa upelelezi kwanza na utaratibu maalum wa uendeshaji wa kesi za udhalilishaji pamoja na dawa za kulevya, hali iliyopelekea kupunguza kwa kiasi kikubwa mrundikano wa kesi mahakamani ambapo katika kipindi hiki, kati ya kesi 19,382 zilizofunguliwa mahakamani, kesi 15,097 zimetolewa uamuzi. Vile vile, Serikali imeongeza idadi ya majaji, mahakimu na makadhi kutoka majaji wanne mwaka 2010 hadi kufikia majaji tisa mwaka 2019, wakiwemo majaji wanawake watatu; mahakimu walikuwa 23 mwaka 2010 na sasa ni 65 na idadi ya makadhi walikuwa sita ambapo wenye shahada walikuwa wawili katika mwaka 2010 na katika mwaka 2019 wapo jumla ya makadhi 14 ambapo walio na shahada ni 8. Watumishi wenye sifa katika Tume ya Kurekebisha Sheria walikuwa 4 na sasa ni 12.

21. **Mheshimiwa Spika,** punguzo la ushuru wa mali maiti kutoka asilimia 5 hadi asilimia 0.25 lililofanywa na Serikali limepelekea wananchi wengi zaidi kumudu kulipia gharama za mirathi ambapo mwaka 2018/2019 tirka 1,365 zenye thamani ya shilingi 24,029,984,312 zilishughulikiwa na kufungwa ikilinganishwa na mwaka 2010/2011 ambapo ni tirka 234 tu zenye thamani ya shilingi 1,531,911,340.35 zilishughulikiwa.

22. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria imefanyia mapitio sheria 37 na kukamilisha sheria 22 zilizowasilishwa katika mamlaka husika. Haya ni mafanikio makubwa ya

kuona kuwa kazi inayofanywa na Tume inakamilika na kuleta tija iliyokusudiwa. Miongoni mwa sheria hizo, Sheria zinazounda taasisi ni tatu, Sheria zinazohusu masuala ya kazi ni nne, Sheria za Usimamizi masuala mbali ni 11, na Sheria zinazohusu usimamizi na uendeshaji wa mashauri ni nne. Aidha, Tume ya Kurekebisha Sheria imefungua maktaba ya kisasa ya sheria inayotoa fursa kwa watendaji kutoka taasisi za sheria kufanya rejea ya masuala ya sheria.

23. **Mheshimiwa Spika,** hali ya majengo yanayotumiwa na Wizara ya Katiba na Sheria imezidi kuimarika katika kipindi hiki ambapo jengo la Wizara lililopo Mazizini, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu, Ofisi ya Mufti, Ofisi Kuu Pemba, Mahakama ya Watoto Mahonda, jengo la usuluhishi Mwanakwerekwe, Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, Ofisi ya Mkoa Mwera, Ofisi ndogo ya Mkurugenzi wa Mashtaka na nyumba ya makaazi ya Muendesha Mashtaka Makunduchi na Mkototoni Kaskazini Unguja yapo katika hali nzuri. Aidha, ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu unaendelea kwa kasi ambapo matarajio ni kulikamilisha katika kipindi cha mwanzo cha mwaka 2020/2021. Majengo yaliyofanyiwa matengezo ni pamoja na Mahakama Kuu Vuga, Mahakama ya Wilaya ya Mkoani, Mahakama ya Kadhi Mwanakwerekwe, Mahakama ya Chake Chake, na Mahakama ya Wilaya Mwanakwerekwe. Matengenezo ya Majengo ya Mahakama na ujenzi wa majengo mapya utaendelea ili kuzifanya taasisi za sheria kuwa na mvuto unaostahiki na wananchi wanaokuja kuhudumiwa wapate hali ya utulivu na stara zaidi.

24. **Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa Sheria ya Mtoto namba 6/2011 umepelekea watoto kupata ulinzi wa kisheria kuhusu mambo ya matunzo, umepunguza migogoro ya kifamilia kuhusu maslahi bora ya mtoto pale wazazi wanapotengana na imewezesha upatikanaji wa fidia kuhusu matunzo ya mtoto. Aidha, kuanzishwa kwa Mahakama ya Watoto kumepelekea kesi za watoto kuendeshwa na kutolewa uamuzi kwa muda mfupi na imesaidia kurekebisha tabia za watoto wanaokinzana na sheria. Vile vile huduma za matunzo kwa watoto katika Vyuo vya Mafunzo zimeimarika.

25. **Mheshimiwa Spika,** katika nchi nyingi za Jumuiya ya Madola, kazi za Sheria hazifanywi na taasisi za Serikali pekee, bali wapo mawakili wa kujitegemea, jumuiya na asasi mbali mbali zilizoundwa kutetea haki za makundi na vile vile, watoa huduma za kisheria katika ngazi ya jamii. Ninayo furaha kulieleza Baraza letu tukufu kuwa Serikali imefanya jitihada kubwa za kuweka zana na nyenzo za kuwezesha vyombo hivi vifanye kazi zao za kuwahudumia wananchi kwa ufanisi zaidi huku zikizingatia miongozo iliyowekwa. Nachukua fursa hii kuipongeza Jumuiya ya Mawakili Zanzibar (ZLS), Mawakili wote wa kujitegemea na Kampuni zao, Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar na Jumuiya ya Majaji Zanzibar na Watoa Huduma za Msaada wa Kisheria kwa ujumla.

MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MALENGO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

26. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa fedha 2019/2020, Wizara ya Katiba na Sheria iliidhinishiwa shilingi 17,551,400,000.00 kwa kazi za kawaida ambapo makadirio ya mishahara yalikuwa shilingi 9,808,386,660.00 na matumizi mengineyo yalikuwa shilingi 7,743,013,303.00. Kiasi cha shilingi 11,657,590,136.00 kilipatikana kwa matumizi ya kawaida, zikiwemo shilingi 7,293,710,182.00 za mishahara sawa na asilimia 74 na shilingi 4,363,879,954.00 za matumizi mengineyo, ambazo ni sawa na asilimia 56. Wizara pia ilipokea jumla ya shilingi 95,000,000.00 kati ya 400,000,000.00 zilizotengwa kutoka Serikalini na shilingi 147,099,000.00 kati ya 1,483,000,000.00 kutoka UNDP za Maendeleo. Jumla ya fedha za maendeleo zilizopatikana ni 242,099,000.00 saa na asilimia 12.8 ya makadirio.

27. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ruzuku Wizara ilikadiriwa kutumia shilingi 2,748,500,000.00 na shilingi 1,565,161,456.00 sawa na asilimia 57 zimepatikana. Kwa upande mwingine, Wizara ilikadiria kukusanya shilingi 792,500,000.00 na kuchangia mapato ya Serikali. Fedha zilizokusanywa ni shilingi 470,229,636.00 sawa na asilimia 59 ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

Mapitio ya Utekelezaji wa Malengo kwa Mwaka 2019/2020

28. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria inasimamia mafungu matano ambayo ni G10 – Wizara ya Katiba na Sheria; G02 – Mahakama; G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka; na G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria ***(kiambatanisho 5a).***

G10 – Wizara ya Katiba na Sheria

29. **Mheshimiwa Spika,** Fungu G10 lina Programu ya Usimamizi wa Katiba na Sheria; Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini na Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara. Yafuatayo ni maelezo kuhusu utekelezaji wa programu hizi tatu ***(kiambatanisho 5b).***

Programu ya Usimamizi wa Katiba na Sheria.

30. **Mheshimiwa Spika,** uratibu wa masuala ya sheria umefanyika ambapo Wizara imetayarisha miswada minne ya sheria na kuiwasilisha katika mamlaka husika. Mikataba mitatu iliyohusu uwekaji wa "UPS" katika jengo la Wizara, mkataba wa kununua gari ya ofisi ya Mufti na mkataba wa kuweka mfumo wa urithishaji kwa njia ya kielektroniki pamoja na mikataba mingine mbali mbali iliyohusu kazi za kitaalamu imetayarishwa. Wizara ilishiriki katika Kamati ya maandalizi ya mkutano wa ushirikiano wa Kisheria wa nchi za Asia na Afrika uliofanyika Dar es salaam na

kushiriki mikutano inayohusu sekta ya sheria na haki za binaadamu iliyohusisha Wizara za Katiba na Sheria za SMT na SMZ. Uratibu wa upatikanaji wa majibu ya hoja za Kamati ya Kudumu ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo ya Baraza la Wawakilishi umefanyika kwa ufanisi ambapo jumla ya Kanuni na Sheria Ndogo ndogo 31 zilizotolewa katika mkutano wa 14, 15 na 16 zilijadiliwa na kutolewa maelekezo.

31. **Mheshimiwa Spika,** dhamana ya kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji wa msaada wa Kisheria imepewa Idara ya Msaada wa Kisheria, ambayo ni idara mpya iliyoanzishwa na Sheria namba 13/2018 chini ya Wizara ya Katiba na Sheria. Utekelezaji wa majukumu ni kama ifuatavyo:-

32. **Mheshimiwa Spika,** mikutano ya kuitambulisha Idara ya Msaada wa Kisheria kwa Watoa huduma za Msaada wa Kishera imefanyika. Ili kukamilisha zana za kufanyia kazi, Kanuni za Msaada wa Kisheria zimetungwa, kutangazwa rasmi katika Gazeti la Serikali na kuanza kutumika. Aidha, Sheria ya Msaada wa Kisheria namba 13/2018 imetafsiriwa kwa lugha nyepesi ya Kiswahili, lengo ni kuwawezesha wananchi kuelewa kwa kina sheria hiyo ambayo ni msingi wa upatikanaji wa msaada wa kisheria kwa watu wasiokuwa na uwezo. Jumla ya nakala 350 za sheria hiyo na vipeperushi 300 vimesambazwa katika maeneo tofauti ya Unguja na Pemba.

33. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea uelewa wananchi kuhusu dhana na fursa za msaada wa kisheria, watoa huduma za msaada wa kisheria 60 na wataka huduma 60 wa Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo yaliyohusu Sheria na Kanuni za Msaada wa Kisheria. Aidha, vikao vya kuwatambulisha wananchi kuwepo kwa huduma za msaada wa kisheria vimefanyika Unguja na Pemba ambapo wananchi 338 wakiwemo wanawake 198 na wanaume 140 wa Unguja (Shehia za Mangapwani, Mahonda, Jambiani Kikadini na Muyuni 'B') na wananchi 150 wa Pemba (Micheweni) walipatiwa mafunzo hayo. Vile vile, mkutano wa robo mwaka wa wahusika wa msaada wa kisheria umeratibiwa na kufanyika, uliowahusisha washiriki 40 (33 kutoka Unguja na saba kutoka Pemba).

34. **Mheshimiwa Spika,** mafanikio zaidi yaliyoweza kupatikana katika kipindi kifupi cha kuweka misingi ya upatikanaji wa msaada wa kisheria ni kuandaliwa kwa mfumo wa usajili kwa njia ya kieliktroniki ambao tayari umeanza kutumika kuwasajili watoaji msaada wa kisheria. Jumla ya Wasaidizi wa Sheria 46 wa Unguja na Pemba wamesajiliwa. Usajili huu ni hatua muhimu ya kuwatambua watoa huduma za msaada wa kisheria na kuiwezesha Serikali kupata takwimu sahihi za huduma wanazozitoa katika jamii. Mfumo huu unapatikana kupitia tovuti ya Wizara ya Katiba na Sheria www.sheriasmz.go.tz.

35. **Mheshimiwa Spika,** maadhimisho ya wiki ya msaada wa kisheria kwa mwaka 2020 yaliyokuwa na Kauli mbiu ya

“Msaada wa Kisheria ni nguzo imara kwa ustawi wa jamii” yamefanyika. Maadhimisho hayo yalikwenda sambamba na Maadhimisho ya Siku ya Sheria Zanzibar. Katika maonesho yaliyoambatana na maadhimisho hayo, jumla ya wananchi 30 wakiwemo wanawake 8 na wanaume 22 wamepatiwa msaada wa kisheria. Shughuli nyingine zilizofanyika katika Wiki ya Msaada wa Kisheria ni pamoja na ziara za utoaji huduma za msaada wa kisheria kwa mahabusu na wanafunzi waliopo Chuo cha Mafunzo maeneo ya Kilimani Unguja na Wete Pemba. Semina zilifanyika katika Shehia za Fukuchani, Kizimkazi Dimbani, Kinyasini Kisongoni na Pwani Mchangani na kuwafikia wananchi 320 wakiwemo wanawake 177 na wanaume 143. Aidha, wananchi na wanafunzi 6,269 wakiwemo wanawake 2,862 na wanaume 3,407 wa Shehia ya Ole, Kiuyu, Maziwa Ngo’mbe, Chuo cha Kiislamu na Waambaa walipatiwa elimu ya msaada wa kisheria. Shughuli hizi zilifanyika kwa ushirikiano na taasisi nyingine za sheria za serikali na zisizo za kiserikali.

36. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha ushirikiano na taasisi nyengine Idara ilishirikiana na taasisi ya Legal Services Facility (LSF) kuandaa mafunzo ya siku tano kwa Wasaidizi wa Sheria kwa upande wa Pemba ili kuwajengea uwezo Wasaidizi wa Sheria juu ya Sheria mbali mbali za Zanzibar, zikiwemo zinazohusu masuala ya ardhi, Mahakama ya Kadhi, mazingira, elimu ya uraia na elimu ya mpiga kura, namna bora ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji, uandishi wa miradi, uhamasishaji jamii,

utatuzi wa migogoro kupitia njia mbadala, umuhimu wa kufanya kazi kwa kujitolea na maadili ya kazi zao.

Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria

37. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti imeratibu matayarisho ya kazi mbali mbali zinazoihusu Wizara. Aidha, kupitia Programu Ndogo hii, maandalizi ya uanzishwaji wa Skuli ya Sheria yamefanyika ikiwemo kupata mahali ambapo Skuli hiyo itaanzia shughuli zake na kufanya matayarisho mengine ya msingi. Skuli ya Sheria Zanzibar imeanzishwa ili kujenga jamii ya wanasheria wenye uweledi na wanaozingatia matakwa ya jamii ya kizanzibari. Skuli hii itawajenga wanasheria wote awamu kwa awamu kuwapatia mafunzo zaidi ya vitendo na kitakuwa ndiyo chombo muhimu cha kuimarisha huduma za kisheria kupitia taaluma na vitendo.

38. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki nyaraka zisizopungua tisa zimetayarishwa na kuwasilishwa katika vikao vya maamuzi ambapo jumla ya nyaraka nane zimefanyiwa maamuzi na kuanza utekelezaji wake. Katika nyaraka hizo upo waraka wa maslahi ya Mahakimu wa Mahakama za Mwanzo, sheria mpya na sheria zilizofanyiwa mapitio nne na kanuni mbili. Aidha, bajeti ya Wizara imetayarishwa na kukamilika. Taarifa na ripoti mbali za Wizara zimeandaliwa na kuwasilishwa katika mamlaka

husika. Utiaji wa betri katika jengo la Wizara umefanyika kwa mafanikio. Hivi sasa vifaa vya kielektroniki kama kompyuta na printa vinavyotumika katika ghorofa nne za jengo vinapata huduma ya umeme wa dharura pindi umeme unapokatika.

39. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji imesimamia miongozo mbali mbali ya kiutumishi ikiwa ni pamoja na uandaaji wa Mkataba wa utowaji wa huduma kwa mtaka huduma ambapo rasimu ya awali imeandaliwa. Kumbukumbu za watumishi zimeimarishwa kwa kuingizwa taarifa zilizokuwa zimekosekana katika mfumo wa kielektroniki. Vile vile, mfumo wa usimamizi wa fedha, ununuzi, habari na ukaguzi wa ndani pamoja na uimarishaji tovuti ya Wizara umesimamiwa ipasavyo.

40. **Mheshimiwa Spika,** katika kuimarisha maslahi ya watumishi program imetoa stahiki mbali mbali za watumishi. Upimaji wa utendaji kazi umeanza kwa utoaji wa majukumu upya kwa watumishi kulingana na nafasi zao walizonazo. Programu hii pia imeendelea kutoa huduma za uendeshaji na utawala zinazojumuisha malipo ya umeme, usafi, matengenezo ya kisima, lifti, matengenezo ya mfumo wa kuzimia moto pamoja na ununuzi wa vifaa vya ofisi na kufanya matengenezo mbali mbali ya vyombo vya usafiri na mashine.

41. **Mheshimiwa Spika,** Program Ndogo ya Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba imeratibu shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba pamoja na ziara za Kamati

ya Baraza la Wawakilishi. Vikao vya watumishi vya ndani ya ofisi na Wakuu wa Taasisi walio chini ya Wizara ya Katiba na Sheria vimefanyika. Aidha, mazingira bora ya kazi pamoja na kuwapatia stahiki zimetolewa.

Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini

42. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini inatekelezwa kupitia Programu Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu unayozihusu Ofisi ya Mufti wa Zanzibar na Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana. Utekelezaji ni kama ifuatavyo:-

Ofisi ya Mufti wa Zanzibar

43. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti wa Zanzibar ina dhamana kisheria ya kuratibu na kusimamia shughuli za Kiislamu zikiwemo kutoa fatwa, kutatua migogoro ya kijamii na kusimamia miongozo kuhusu masuala ya kidini. Katika kipindi hiki, misikiti 173 na madrasa 233 imesajiliwa na kukaguliwa kwa madhumuni ya kuwakumbusha walimu wa madrasa na Maimamu juu ya wajibu wa kudhibiti na kupambana na mmong'onyoko wa maadili uliojitokeza ndani ya jamii yetu. Aidha, walimu 31 wa madrasa wamepatiwa mafunzo ya kutumia muongozo wa njia bora za kuadabisha. Vile vile, jumla ya migogoro 181 inayohusiana na ndoa, misikiti, mirathi, na madrasa imepokelewa na kupatiwa ufumbuzi. Sambamba na hayo maswali 343 yanayohusiana na talaka na ndoa yamejibiwa

kwa kupatiwa ufumbuzi na wananchi 196 wamekamilisha na kupewa vyeti kwa kuhitimu mafunzo ya ndoa na 85 wamesitishwa kuendelea na mafunzo hayo kutokana na mripuko wa homa ya mafua makali (korona).

44. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imeendelea kutatua migogoro ya kidini pamoja na kusimamia na kuratibu vikao vya kamati ya kitaifa ya kuthibitisha kuandama kwa mwezi. Vile vile, Ofisi imeendeleza utaratibu wake wa kufanya ziara kwa baadhi ya misikiti na madrasa. Ofisi pia imeendelea kuimarisha mahusiano na taasisi za nje na ndani ya nchi, uhamasishaji wa amani na utulivu nchini na kujibu masuala mbali mbali ya waumini.

45. **Mheshimiwa Spika,** vipindi vya mawaidha ya dini ya Kiislamu kupitia ZBC redio na ZBC televisheni vinavyohusu ndoa, talaka, maradhi ya korona, uhusiano mwema katika jamii vimetolewa na vipidi 107 vimerushwa hewani vikiwemo vya masuali na majibu ya Dini ya Kiislamu.

46. **Mheshimiwa Spika,** katika kuwajengea uwezo watumishi, Ofisi imewapeleka masomoni watumishi wawili kwa ngazi ya shahada. Aidha vikao 4 vya kuthibitisha kuandama kwa mwezi vimeratibiwa na kulipia huduma za uendeshaji wa ofisi.

Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

47. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana imeendelea kuimarisha kazi na kusimamia Mirathi ya Waislamu, Mali za Wakfu, Amana, Hijja, Sala

na Mabaraza ya Iddi kitaifa, zakka, na misaada ya kheri. Katika mwaka 2019/2020 Kamisheni ilijipanga kutoa huduma na kufanikisha utekelezaji wa malengo yake kama ifuatavyo: -

48. **Mheshimiwa Spika,** katika urithishaji wa mali, tirka 838 zimefunguliwa, tirka 564 zenye thamani ya shilingi 21,965,373,633.40 zimefungwa na warathi kupewa haki zao na tirka 253 zinaendelea kushughulikiwa. Aidha, Kamisheni imetoa ushauri wa kisheria kwa mashauri 90 ambapo mizozo 61 kati ya hiyo 23 imepatiwa ufumbuzi, 38 inaendelea kushughulikiwa na saba imepelekwa mahakamani. Katika kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu, kazi ya kuingiza taarifa imeanza ambapo majalada ya miaka miwili (2001 na 2002) yameingizwa katika mfumo wa kielektroniki. Vile vile, hatua za awali za kuanzishwa mfumo wa kielektroniki wa shughuli za mirathi zimeanza.

49. **Mheshimiwa Spika,** utunzaji, usimamizi na uimarishaji wa kumbukumbu za Mali za Wakfu na Amana umeendelea. Nyumba zote 412 na mashamba 23 sawa na asilimia 100 yamekaguliwa. Nyumba 97 zipo katika hali nzuri, 16 wastani na 12 zinahitaji matengenezo makubwa. Pia nyumba 22 zimefanyiwa matengenezo, ambapo saba zimefanyiwa matengenezo makubwa na 15 zimefanyiwa matengenezo madogo yaliyogharimu shilingi 432,700,660. Kodi ya shilingi 343,309,140 sawa na asilimia 70 imekusanywa na taarifa za mali za wakfu zimeendelea kuingizwa katika mfumo.

50. **Mheshimiwa Spika,** Sala na Baraza la Idd el Hajj kitaifa limeratibiwa na kufanyika katika Wilaya ya Magharibi A. Sala ilisaliwa Katika Viwanja vya Chuo cha Ualimu Nkurumah na Baraza la Iddi lilifanyika katika viwanja vya Mpira Dole. Nachukua fursa hii kulifahamisha Baraza lako Tukufu kuwa shughuli za Usimamizi wa Sala na Mabaraza ya Iddi zitakuwa zinasimamiwa na Ofisi ya Mufti wa Zanzibar kulingana na marekebisho ya Sheria ya Ofisi ya Mufti.

51. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka 2019 (1440) Kamisheni iliendelea kuratibu shughuli za Hijja ambapo jumla ya mahujaji 2,592 walisafirishwa na Taasisi 22 za Zanzibar na taasisi 15 za Tanzania Bara. Mahujaji wote walirejea Tanzania salama isipokua mmoja aliefariki Uwanja wa Ndege wa Zanzibar. Maandalizi ya Hijja ya Mwaka 2020 (1441 Hijria) yanaendelea licha ya hali tete iliyoikumba Dunia. Aidha, hatua za uanzishaji wa Mfuko wa Hijja zinaendelea ambapo kwa sasa Kanuni za Hijja zipo hatua ya kuchapishwa ***(viambatanisho 8a&b vinahusika).***

52. **Mheshimiwa Spika,** wananchi 38 wamenufaika na zakka ya shilingi 14,000,000 wengi wakisaidiwa katika kuanzisha biashara na kulipa madeni. Misaada ya kheri yenye thamani ya shilingi 519,000,000 imekusanywa na kugawiwa kwa wananchi wa Unguja na Pemba mjini na vijijini. Vile vile, Kamisheni imekaa vikao na taasisi zinazojishughulisha na masuala ya zakka na misaada ili kuratibu vyema shughuli hiyo na kupata mafunzo ya mbinu mpya za kuendesha shughuli za zakka kutoka taasisi mbali mbali duniani.

53. **Mheshimiwa Spika,** uelimishaji ni jambo linalopewa kipaumbele katika kufanikisha majukumu ya Kamisheni. Jumla ya Vipindi 14 vya Redio na nane vya TV vimerushwa hewani. Aidha, semina tatu za uelimishaji wa taratibu za Mirathi na majukumu ya Kamisheni zimefanyika kwa Masheha wa Wilaya za Kaskazini A na B, Wilaya ya Kusini na Wilaya ya Kati na kugawa vipeperushi 1,900.

54. **Mheshimiwa Spika,** Kamisheni inaendelea na taratibu za kuhamishia Wilayani huduma inazozitoa kwa lengo la kuwasogezea wananchi huduma, katika hili tayari wanaotarajiwa kufanyakazi katika maeneo hayo wameshafanyiwa usaili na mara taratibu za uajiri zikikamilika huduma zetu zitaanza kupatikana katika Wilaya za Kaskazini A na B, Kati na Kusini kwa Unguja, Micheweni na Mkoani kwa Pemba.

Upatikanaji wa Fedha kwa Fungu G10

55. **Mheshimiwa Spika,** Fungu G10 katika mwaka 2019/2020, Fungu G10 lilikadiriwa kutumia shilingi 2,514,200,000.00 zilizotengwa kwa ajili ya matumizi ya kawaida zilihusisha shilingi 1,250,200,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,264,000,000.00 za matumizi mengineyo. Shilingi 1,633,659,971.00 sawa na asilimia 65 zimepatikana. Kati ya fedha hizo shilingi 951,353,882.00 sawa na asilimia 76 ni mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 682,306,089.00 sawa na asilimia 54 ni matumizi mengine.

56. **Mheshimiwa Spika,** fedha za ruzuku zilizotengwa kwa ajili ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ni shilingi 1,092,200,000.00, zikiwemo shilingi 582,100,000.00 kwa ajili ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 510,100,000.00 kwa matumizi mengineyo. Shilingi 766,699,724.00 sawa na asilimia 70 zimepatikana. Kati ya fedha hizo shilingi 399,931,790.00 sawa na asilimia 69 ni mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 366,767,934.00 sawa na asilimia 72 ni matumizi mengine. Fungu hili (kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana) lilikadiriwa kuchangia shilingi 82,190,000.00 katika Mfuko Mkuu wa Serikali ambapo shilingi 52,608,374.00 (64%) zimepatikana ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

Taasisi Zinazojitegemea za Wizara

57. **Mheshimiwa Spika,** Wizara ya Katiba na Sheria ina taasisi nne zenye mafungu yanayojitegemea. Kila Fungu lina programu mbili. Programu ya kwanza inahusu utekelezaji wa kazi za msingi za taasisi na programu ya pili inahusu utawala na uendeshaji wa ofisi. Fedha zilizomo katika programu hizi zinasimamiwa na Wakuu wa Taasisi husika.

G02 – Mahakama

58. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama ina jukumu la kutafsiri sheria, kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya jinai na madai yanayowasilishwa mahakamani. Katika kufanikisha jukumu hilo Mahakama imeweza

kusikiliza kesi mbali mbali za madai na jinai pamoja na kuratibu rufaa za Mahakama Kuu. Kwa kipindi cha Julai 2019 hadi Machi 2020 Mahakama imepokea na kusajili kesi 7,289 kutoka mahakama zote Unguja na Pemba.

59. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hicho, Mahakama Kuu imepokea mashauri mapya 63 ikijumuishwa na mashauri 90 ya nyuma na kufanya jumla ya mashauri 153. Kati ya mashauri hayo, mashauri matatu yametolewa uamuzi. Katika Kitengo cha Mahakama ya Kazi maombi 31 yamefunguliwa na kufanya Mahakama hiyo iwe na maombi 53 kwa kujumuisha na maombi 22 yaliyosajiliwa kabla. Hakuna maombi yaliyotolewa uamuzi. Mahakama ya Biashara imepokea mashauri mapya sita ukijumuisha na mashauri matano ya nyuma na kuwa na jumla ya mashauri 11. Mashauri hayo bado yanaendelea kusikilizwa. Katika Mahakama za Mikoa, mashauri mapya 879 yamepokelewa na kufanya Mahakama hizo ziwe na jumla ya mashauri 1,605 yakijumuishwa na mashauri mengine 726 yaliyosajiliwa kabla. Mahakama za Mikoa zimetolea uamuzi mashauri 198.

60. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama za Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,445 na kufikisha jumla ya mashauri 2,142 yakijumuishwa na mashauri 697 yaliyosajiliwa kabla. Katika kipindi hiki Mahakama hizo zimetoa uamuzi kwa mashauri 995. Kwa upande wa Mahakama za Mwanzo, mashauri mapya 3,128 yamepokelewa na kufikisha jumla ya mashauri 3,639 yakijumuishwa na mashauri 511

yaliyosajiliwa kabla ambapo mashauri 2,745 yametolewa uamuzi. Mahakama ya Rufaa ya Tanzania nayo katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilipokea mashauri 16. Kati ya mashauri hayo, 15 yalitolewa uamuzi na shauri moja bado linaendelea.

61. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa Mahakama ya Kadhi wa Rufaa mashauri mapya 53 yamepokelewa na kufanya jumla ya mashauri 95 yakijumuishwa na mashauri 46 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 14 kati ya hayo yametolewa uamuzi. Aidha, Mahakama za Kadhi wa Wilaya zilipokea mashauri mapya 1,412 na kufikisha jumla ya mashauri 2,226 yakijumuishwa na mashauri 814 yaliyosajiliwa kabla. Mashauri 836 yametolewa uamuzi. Kwa upande wa Mahakama za Watoto, mashauri mapya 144 yalipokelewa na kufikisha jumla ya mashauri 322 yanapojumuishwa na mashauri 178 yaliyosajiliwa kabla ambapo mashauri 24 yametolewa uamuzi.

62. **Mheshimiwa Spika,** kwa uchambuzi huo, Mahakama imepokea na kusajili jumla ya mashauri 7,289 kutoka Mahakama zote kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 ambapo idadi ya mashauri yaliyosikilizwa na kutolewa uamuzi ni 4,834 sawa na asilimia 66.3 ***(viambatanisho 6a, b&c vinahusika).***

63. **Mheshimiwa Spika,** ujenzi wa jengo jipya la Mahakama Kuu Tunguu unaendelea na matarajio ni kukamilika kwa wakati uliopangwa. Aidha, Mahakama imewapatia

mafunzo elekezi watumishi wapya 62, wa Unguja na Pemba kupitia Chuo cha Utawala wa Umma pia watumishi 255 wa Mahakama Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo ya ndani yakiwemo mafunzo ya Sheria ya Usimamizi wa Mahakama namba 11/2018, mapambano ya rushwa na athari zake, uandishi wa mikataba, takwimu na uandishi wa sheria. Majaji watatu na mahakimu watatu walihudhuria mafunzo mafupi nchini Afrika ya Kusini, India na China kwa lengo la kuimarisha utendaji wa kazi. Aidha, viongozi wa Mahakama wameshiriki mikutano ya kimataifa ya Majaji Wakuu Duniani uliofanyika nchini India, na ule wa Majaji Wakuu kwa Nchi za Kusini mwa Afrika uliofanyika nchini Shelisheli na Misri. Makadhi na Watendaji Waandamizi wa Mahakama ya Kadhi wamepatiwa mafunzo juu ya uendeshaji kesi na haki za binaadamu pamoja na kushiriki mafunzo mafupi ya uendeshaji kesi nchini Saudi Arabia.

64. **Mheshimiwa Spika,** Mkutano wa Majaji na Mahakimu wa Afrika Mashariki (EAMJA) ulifanyika hapa Zanzibar na kuwakutanisha pamoja Majaji na Mahakimu kutoka Tanzania, Kenya, Uganda, Rwanda, Mahakama ya Afrika Mashariki na mwenyeji Zanzibar. Kauli mbiu ya mkutano huo ilikua ni Land & Environment for Sustainable Economic Develeopment in East Africa. Katika mkutano huo, pamoja na mambo mengine, changamoto katika sekta ya ardhi na mazingira na namna ya kuzitafutia ufumbuzi zilijadiliwa. Aidha, Mahakama imeadhimisha Siku ya Sheria Zanzibar iliyokuwa na Kaulimbiu “Dumisha Demokrasia na Utawala wa Sheria katika Uchaguzi Mkuu 2020”. Maadhimisho

hayo yalifana sana na yalitoa fursa kwa wananchi kujifunza na kujipatia huduma za sheria.

65. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Utumishi wa Mahakama ikiwa na jukumu lake la kusimamia ajira, nidhamu na maslahi ya kiutumishi kwa watumishi wa Mahakama, iliendelea na taratibu zake za vikao ambapo vikao viwili vilifanyika. Aidha, Tume ya Utumishi ya Mahakama imefanya ziara katika Mahakama za Unguja na Pemba kwa lengo la kuzungumza na watumishi na kusikiliza changamoto za kiutumishi zinazowakabili. Wajumbe wa Tume ya Utumishi ya Mahakama wamepatiwa semina elekezi ya utendaji na utekelezaji na majukumu yao.

66. **Mheshimiwa Spika,** katika mwaka wa Fedha 2019/2020 Mahakama iliidhinishiwa shilingi 7,849,900,000.00 ambapo Mahakama pekee iliidhinishiwa kutumia Shilingi 6,214,400,000.00. Kati ya hizo shilingi 4,411,100,000.00 ni kwa ajili ya mishahara na stahiki na shilingi 1,803,300,000.00 kwa matumizi mengineyo. Katika kipindi hiki Mahakama iliingiziwa shilingi 4,848,064,002.00 (78%) ambapo fedha za mishahara zilikuwa shilingi 3,407,352,355.00 (77%) na matumizi mengineyo shilingi 1,440,711,647.00 (80%). Mahakama ya Kadhi iliidhinishiwa ruzuku ya shilingi 1,635,500,000.00 kutoka serikalini ambapo kati ya fedha hizo, shilingi 838,686,660.00 za mishahara na stahiki na shilingi 796,813,343.00 za matumizi mengineyo. Mahakama ya Kadhi iliingiziwa shilingi 784,595,068.00 (48%) ambapo shilingi 616,759,290.00 (74%) zilitumika

kwa Mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 167,835,778.00 (21%) kwa matumizi mengineyo. Aidha, shilingi 710,310,000.00 zilikadiriwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali. Shilingi 417,621,262.00 (59%) zimekusanywa na kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

67. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu ni miongoni mwa Ofisi zinazojitegemea ambayo imeanzishwa kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Kifungu cha 55 na 56 cha Katiba kimeeleza kuwepo kwa Mwanasheria Mkuu na majukumu yake. Aidha, Sheria namba 6/2013 inapambanua zaidi kazi za Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Mwanasheria Mkuu ndiye Mshauri Mkuu wa Serikali kwa mambo yote ya kisheria. Katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria Ofisi inafanya kazi mbali mbali za kisheria ikiwa ni pamoja na kutoa ushauri wa kisheria kwa taasisi mbali mbali za Serikali, uandishi wa miswada ya sheria, kanuni na matangazo ya kisheria. Kusimamia kesi na mashauri ya madai kwa niaba ya Serikali, kuandaa hati na nyaraka za kisheria, kutoa huduma za ushauri na kusimamia mikataba ambayo Serikali ni sehemu ya mikataba hiyo pamoja na kufanya mambo mengine ya kisheria yatakayoletwa na Serikali.

68. **Mheshimiwa Spika,** katika kuhakikisha inafanya kazi kwa ufanisi na kufikia malengo, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu

imeongeza nafasi za watendaji kutoka watumishi 51 hadi kufikia watumishi 77 (Ongezeko la asilimia hamsini). Ni matarajio ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu kuongeza ufanisi na kuongeza wigo wa kutoa huduma za ushauri kwa taasisi za Serikali kwa wakati. Aidha, Ofisi imeimarisha utendaji kwa kufungua Ofisi Pemba. Hii inatokana na haja ya muda mrefu ya kuanzishwa kwa Ofisi hiyo kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ikiwemo ongezeko la Mashauri ya Madai kutoka Pemba. Hivyo Ofisi tayari imefunguliwa na Mawakili wa Serikali wenye uzoefu wamehamishiwa katika ofisi hiyo tokea mwanzoni mwa mwezi wa Machi mwaka huu.

69. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mwanasheria Mkuu bado imeendelea na utoaji wa elimu kwa jamii katika maeneo ya shehia za Unguja na Pemba kwa nia ya kuelimisha umma kuhusiana na masuala mbali mbali kama Sheria za ardhi na vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia. Suala la kuandaa Miswada ya Sheria ni moja kati ya jukumu la msingi la Ofisi ya Mwanasheria Mkuu katika kutekeleza hilo na kuimarisha mfumo wa Sheria za Zanzibar kwa mwaka 2019/2020 Ofisi imeandaa Miswada 16 ya sheria ambayo imewasilishwa Baraza la Wawakilishi kwa kujadiliwa na hatimae kupitishwa. Kati ya hiyo Miswada minane imeshawekwa saini na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na kuwa Sheria. Aidha, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeandaa Kanuni 15 zinazotokana na sheria tofauti kwa lengo la kuzifanya sheria hizo ziweze kutekelezeka kwa ufanisi

zaidi. Matangazo ya kisheria 44 yalifanyiwa kazi mwaka huu ***(kiambatanisho 7a &b kinahusika).***

70. **Mheshimiwa Spika,** katika suala la usimamizi wa mikataba, Ofisi imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kazi ya kuishauri Serikali juu ya masuala mbali mbali ambayo Serikali ilihitaji kufunga nayo Mikataba. Jumla ya rasimu za mikataba 317 zimefanyiwa mapitio na kutolewa ushauri na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu. Rasimu za mikataba hiyo zinajumuisha ushauri elekezi (consultancy), huduma (goods and services), ujenzi (Works), kodi (Leases) na ushirikiano (Joint ventures). Aidha, jumla ya hati za maelewano (MoU) 51 zinazohusu Sekta ya Elimu, Afya, Ujenzi, Biashara, Uchumi, Kilimo na Uvuvi zilifanyiwa mapitio na kutolewa ushauri.

71. **Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa kuiwakilisha Serikali kwenye mashauri ya kesi na kutoa ushauri wa kisheria kuhusiana na mashauri hayo kwa mwaka 2019/2020 Ofisi imesimamia jumla ya kesi 115, katika kesi hizo kesi 14 zimefikia hatua ya kutolewa uamuzi ambapo kati ya hizo Serikali imeshinda kesi tano za Mahakama ya Rufaa na kesi Tisa za Mahakama Kuu. Kwa sasa kesi 101 zinaendelea kusimamiwa zikiwa katika hatua mbali mbali. Kwa upande wa Utawala na Usimamizi wa Fedha Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kutekeleza wajibu wake kwa kusimamia vyema watendaji na kuhakikisha wanatekeleza majukumu yao kwa ufanisi na kuimarisha mazingira bora ya kazi, kuwapatia vitendea kazi na stahiki zao pamoja na kuwajengea uwezo.

72. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi imewajengea uwezo watumishi wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu. Watumishi wawili wamesomeshwa katika ngazi ya shahada ya pili ya sheria na mtumishi mmoja katika ngazi ya shahada ya kwanza ya sheria. Vile vile, mawakili wa Serikali wapatao 35 wamepatiwa mafunzo ya utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi na athari za kimazingira. Aidha, watendaji wa kada mbali mbali wapatao watano wamepatiwa mafunzo ya muda mfupi ndani na nje ya nchi ili kuleta ufanisi na kujifunza mbinu mpya za kazi. Vile vile, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu imeendelea kuimarisha mazingira ya kazi kwa kununua vitendea kazi zikiwemo samani za ofisi, vitabu na vipando ili kurahisisha utendaji kwa watumishi. Aidha, Ofisi imewapatia watendaji waliohamishiwa Pemba nyumba ya makaazi pamoja na samani ili kuwaondoshea usumbufu na kuweza kutekeleza majukumu yao kwa uhakika na ufanisi zaidi.

73. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iliidhinishiwa shilingi 2,114,300,000.00 zikiwemo shilingi 736,400,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 1,377,900,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana kufikia Machi 2020 ni shilingi 1,291,268,695.00 sawa na asilimia 61 kati ya fedha hizo 593,314,395.00 sawa na asilimia 81 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 697,954,300.00 sawa na asilimia 51 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).***

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

74. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka ilianzishwa mwaka 2002 chini ya kifungu 56A cha Katiba kupitia Marekebisho ya Nane ya Katiba ya Zanzibar. Kazi kuu ya Ofisi ni kuendesha mashtaka ya jinai mbele ya mahakama zote za sheria, isipokuwa mahakama za kijeshi kwa kosa lililofanywa katika Zanzibar.

75. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka imetekeleza kazi za kawaida kwa ufanisi. Jumla ya kesi za jinai 2,503 zimefunguliwa katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba. Kesi 1,387 zimetolewa uamuzi na kesi 1,116 zinaendelea katika hatua tofauti. Kadhalika, ushirikiano umeimarishwa baina ya Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka na taasisi nyengine zinazohusika na masuala ya jinai kama vile Mahakama, Magereza, Jeshi la Polisi, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi ili kuhakikisha usimamizi bora wa haki za jinai kwa wananchi.

76. **Mhesimiwa Spika,** Ofisi imewapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wanne katika kada ya sheria ngazi ya shahada ya uzamili. Kati ya hao wawili ni wanaume na wawili ni wanawake. Jumla ya wanasheria 12 walihudhuria mafunzo mbali ya muda mfupi ambayo yameongeza ujuzi na taaluma ya kutekeleza vyema majukumu ya kazi za Ofisi.

77. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliidhinishiwa shilingi 2,869,500,000.00 zikiwemo shilingi 1,669,900,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na shilingi 1,199,600,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana ni shilingi 1,603,694,875.00 sawa na asilimia 56. Kati ya fedha hizo 1,074,235,250.00 sawa na asilimia 64 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 529,459,625.00 sawa na asilimia 44 kwa matumizi mengineyo. Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kilitengewa ruzuku ya shilingi 20,800,000.00 na fedha zilizopatikana ni shilingi 13,866,664.00 sawa na asilimia 67. Aidha Kituo cha Mafunzo ya Sheria kilikusanya shilingi 80,000,000.00 ***(viambatanisho nam. 1&3 vinahusika).***

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

78. **Mheshimiwa Spika,** Tume ya Kurekebisha Sheria imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kukamilisha mapitio ya Sheria sita, ambazo ni Sheria ya Matumizi ya Ardhi namba 12/1992, Sheria ya Mahakama ya Ardhi namba 7/1994, Sheria ya Upimaji Ardhi namba 9/1990, Sheria ya Kamisheni ya Ardhi namba 6/2015, Sheria ya Usajili wa Wathamini namba 5/2015 na Sheria ya Utambuzi wa Ardhi namba 8/1990.

79. **Mheshimiwa Spika,** utafiti na uchambuzi wa matumizi ya Sheria za Zanzibar umefanyika ambapo Tume ilijiwekea

lengo la kuzifanyia utafiti jumla ya Sheria 88 ambapo hadi kufikia Machi 2020, sheria 66 zilifanyiwa uchambuzi ili kugundua uimara, upungufu na matumizi ya sheria hizo. Kukamilika kwa kazi hii kutasaidia sana kuweka mpango endelevu wa mapitio ya Sheria za Zanzibar.

80. **Mheshimiwa Spika,** vipindi 35 vimerushwa hewani ili kutoa uelewa juu ya kazi za Tume na umuhimu wa mapitio ya sheria. Aidha, Tume imefanya mkutano na Waandishi wa Habari kwa lengo la kufafanua nafasi ya vyombo vya habari katika kuelimisha jamii kuhusu Sheria na namna zinavyoathiri maisha yao ya kila siku. Kwa mnasaba huo huo wa kujenga uelewa, Tume imechapisha na kusambaza vipeperushi 2,000 kwa wananchi Unguja na Pemba. Aidha, Tume imetoa mafunzo kuhusu Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa watumishi wake.

81. **Mheshimiwa Spika,** katika kipindi hiki Tume imewapatia mafunzo wanasheria tisa na afisa mipango mmoja kuhusiana na mbinu za kufanya utafiti wa kisheria na uandaaji wa ripoti za mapitio ya Kisheria. Katika kuimarisha mashirikiano ya Kimataifa kikanda na Kitaifa, watendaji wawili wa Tume walifanya ziara ya kikazi ya siku nne kwa lengo la kujifunza na kubadilishana uzoefu na watendaji wa Tume ya Kurekebisha Sheria ya Mauritius. Ziara hiyo imesaidia sana katika kupata uzoefu na kuimarisha mashirikiano na Taasisi zinazofanyakazi sawa na Tume.

82. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa Fedha 2019/2020 Tume ya Kurekebisha Sheria iliidhinishiwa shilingi 1,090,500,000.00 zikiwemo shilingi 320,000,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 770,500,000.00 kwa matumizi mengineyo. Jumla ya fedha zilizopatikana kufikia Machi 2020 ni shilingi 715,741,137.00 sawa na asilimia 66. Kati ya fedha hizo shilingi 250,763,220.00 sawa na asilimia 78 ni kwa malipo ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 464,977,917.00 sawa na asilimia 60 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 1 kinahusika).***

MUELEKEO WA PROGRAMU ZA WIZARA YA KATIBA NA SHERIA KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021

83. **Mheshimiwa Spika,** baada ya kutoa maelezo ya utekelezaji wa bajeti ya Wizara yangu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 sasa naomba kutoa maelezo ya muelekeo wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Vipaumbele vya Wizara ya Katiba na Sheria kwa mwaka 2020/2021

84. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Wizara ya Katiba na Sheria imejipangia kutekeleza vipaumbele vifuatavyo:-

1. Kuendeleza kuimarisha majengo ya Wizara yakiwemo ya Mahakama. Katika mwaka wa fedha 2020/2021 Wizara inatarajia kukamilisha ujenzi wa

Mahakama Kuu Tunguu, kuanza ujenzi wa Skuli ya Sheria, Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti na kufanya matengenezo ya majengo ya mahakama ya Wete, Konde na Mkokotoni;

2. Kuendeleza jitihada zilizoanza za kutoa huduma za msaada wa kisheria katika ngazi ya jamii pamoja na kuanza kazi kwa Skuli ya Sheria Zanzibar. Jitihada zaidi zitafanywa za kutafsiri sheria mbali mbali kwa lugha nyepesi ya Kiswahili;
3. Kuendelea kuimarisha utendaji katika taasisi za sheria;
4. Kuimarisha usimamizi wa mashauri ya madai na kufanya mapitio ya sheria. Aidha, Usimamizi wa mashauri ya jinai katika ngazi ya mkoa utaendelezwa;
5. Kusimamia na kuratibu shughuli za fatwa, mashauri, ushauri wa kidini, taaluma, tafiti, misikiti na madrasa;
6. Kuendelea kuimarisha uhifadhi wa kumbukumbu za mali za wakfu na amana, kuimarisha huduma na mfuko wa hijja na kutekeleza upelekaji huduma za Kamisheni ya Wakfu Wilayani; na
7. Kuimarisha uratibu wa masuala ya sheria.

G10 – Wizara ya Katiba na Sheria

85. **Mheshimiwa Spika,** katika utekelezaji wa program hii, yafuatayo yatatekelezwa:-

Programu: Usimamizi wa Katiba na Sheria

86. **Mheshimiwa Spika,** kupitia Programu hii, masuala ya sheria yataendelea kuratibiwa likiwemo suala la uratibu sheria ndogo ndogo na kanuni ili kuhakikisha kuwa zana hizi zinakamilika na kutumika ipasavyo. Aidha, ushirikiano na Wizara ya Katiba ya Serikali ya Muungano wa Tanzania na nchi nyingine utaendelea kuimarishwa.

87. **Mheshimiwa Spika,** Idara ya Msaada wa Kisheria imejipanga kuendelea na jukumu lake kuu la kuratibu, kuendesha na kusimamia utoaji msaada wa kisheria. Katika kipindi hiki Idara itaendelea kuwasajili na kuwafanyia ukaguzi watoaji msaada wa kisheria, kuandaa utafiti juu ya changamoto za upatikanaji wa msaada wa kisheria, kutoa elimu ya sheria kwa wananchi, kufanya maadhimisho ya wiki ya msaada wa kisheria na kuendesha mafunzo ya ushajihishaji wa utatuzi wa migogoro kupitia njia mbadala. Aidha, Idara itaendelea na vikao vya robo mwaka vya wahusika wa msaada wa sheria, kukamilisha ripoti ya mwaka ya msaada wa kisheria na kuandaa Jarida la Msaada wa Kisheria kwa lengo la kutoa elimu zaidi kwa wananchi. Vile vile, Idara itawajengea uwezo watendaji wake kwa kuwapatia mafunzo ya muda mfupi na kufanya

ziara za kujenga mahusiano na mashirikano kwa taasisi zenye malengo sawa na Idara.

Programu: Usimamizi wa Masuala ya Dini

88. **Mheshimiwa Spika,** Ofisi ya Mufti wa Zanzibar imepanga kusajili misikiti na madrassa na kufanya ukaguzi, kutatua migogoro, kutoa mafunzo kwa masheikh, kuandaa vipindi vya dini, kuandaa Baraza la Iddi na kuratibu ushirikiano wa kitaifa na wa kikanda kwa jumuiya za kiislamu. Vile vile, Ofisi itasimamia na kuendeleza misikiti ya kitaifa, kufanya na kuratibu vikao vya Baraza la Ulamaa pamoja na vikao vya kuandama kwa mwezi, kukusanya fatwa mbali mbali zinazotolewa na masheikh na kuimarisha shughuli za kiofisi.

89. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana inakusudia kuendelea kuimarisha Huduma za Mirathi, Wakfu na Amana kwa kuimarisha huduma zake katika Wilaya za Kaskazini A na B, Kusini na Kati kwa Unguja, na Mkoani na Micheweni kwa Pemba; kuimarisha Huduma za Hijja na Mfuko wa Hijja ili wananchi wengi zaidi waweze kutekeleza wajibu wao huo na kupanua wigo wa ukusanyaji wa zakka ili kusaidia kuinua uchumi kwa wananchi wa kipato cha chini.

Programu: Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria.

90. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria ina programu ndogo tatu na inatekelezwa kupitia Idara ya Utawala na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Utafiti na Ofisi Kuu – Pemba.

91. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji imepanga kufanya mapitio ya mpango wa rasilimali watu wa Wizara, kubainisha changamoto za utekelezaji na kuweka malengo yenye uhalisia na kuimarisha mazingira ya kazi kwa watumishi kwa ununuzi wa vifaa na matengenezo ya miundombinu. Aidha, Programu itaendelea kuwezesha mikutano mbali mbali ya wizara ikiwemo ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalam, na kuimarisha zana za kufanyia kazi kulingana na maelekezo ya Ofisi Kuu ya Utumishi wa Umma. Aidha, program itawezesha shughuli za Bodi ya Zabuni, Ukaguzi wa Ndani, zikiwemo ziara za kikazi za Wakaguzi wa Ndani kisiwani Pemba, kuratibu utekelezaji wa masuala ya mtambuka, uhusiano na taasisi mbali mbali, ikiwemo Serikali ya Muungano wa Tanzania na kuendeleza matukio mbali mbali yanayohusu sekta ya sheria, ikiwemo michezo.

92. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti itatayarisha Mpango Mkakati wa Wizara (2020 – 2025) na kusimamia utekelezaji wake. Aidha, Idara itaendelea kuratibu ushirikiano wa kiutendaji

baina ya Wizara ya Katiba na Sheria ya SMZ na Wizara ya Katiba na Sheria ya SMT na kusimamia miradi iliyopangwa kutekelezwa katika Wizara na Taasisi zake. Idara pia itaendelea kuimarisha ukusanyaji, uhifadhi, usimamizi na matumizi ya Takwimu za Wizara na kuwajengea uwezo watendaji katika uandaaji wa mipango inayozingatia matokeo ya utoaji huduma kwa wananchi. Idara pia itaendelea kukamilisha mapitio ya nyaraka mbali mbali zinazohitajika katika usimamizi wa masuala ya katiba na sheria. Katika kipindi kijacho pia Idara itahakikisha tija zaidi inapatikana katika utekelezaji wa shughuli za Kamati za Baraza la Wawakilishi zinazofuatilia utendaji wa Wizara ya Katiba na Sheria ili ufanisi zaidi uweze kupatikana.

93. **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo ya Uratibu Shughuli za Wizara Pemba itaendelea kutekeleza shughuli zote za Wizara zinazotekelezwa Pemba, kusimamia na kuratibu shughuli za kitaifa zinazoihusu Wizara ya Katiba na Sheria zinazotekelezwa Pemba na kushirikiana na watoa huduma za sheria walioko Pemba katika kufikisha huduma zao kwa wananchi. Aidha, Programu hii itaendelea kuwajengea uwezo watumishi na kuweka mazingira mazuri ya kazi. Katika kipindi hiki cha kuelekea Uchaguzi Mkuu, Ofisi Kuu Pemba kwa kushirikiana na taasisi za sheria na vyombo vingine vinavyohusika itahakikisha kuwa inasimamia vyema utawala wa sheria katika masuala yanayoihusu Wizara ya Katiba na Sheria.

Maombi ya Fedha kwa Ajili ya Fungu G10

94. **Mheshimiwa Spika,** ili kuliwezesha Fungu G10 liweze kutekeleza majukumu yake naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 8,076,700,000.00. Kati ya fedha hizo, shilingi zipo shilingi 5,022,700,000.00 kwa matumizi ya kawaida kwa mchanganuo ufuatao: Jumla ya shilingi 3,273,600,000.00 ni za mishahara shilingi 1,308,300,000.00 na matumizi mengineyo shilingi 1,965,300,000.00; ruzuku ya shilingi 1,749,100,000.00, kwa ajili ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Skuli ya Sheria Zanzibar. Kati ya fedha hizo za ruzuku, shilingi 1,229,100,000.00 (mishahara 545,800,000.00 na matumizi mengineyo 683,300,000.00) ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana na Shilingi 520,000,000.00 (mishahara 70,000,000.00 na matumizi mengineyo 450,000,000.00) kwa ajili ya Skuli ya Sheria; na shilingi 3,054,000,000.00 za maendeleo zikiwemo shilingi 1,500,000,000.00 kutoka serikalini na shilingi 1,554,000,000.00 kutoka kwa washirika wa maendeleo (UNDP). Aidha, Fungu G10 linakadiria kukusanya na kuchangia katika Mfuko Mkuu wa Serikali shilingi 55,700,000.00 zitakazokusanywa kupitia Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana ***(viambatanisho 2,3, &4).***

G02 – Mahakama

Programu: Upatikanaji wa Haki na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

95. **Mheshimiwa Spika,** Mahakama imejipangia kuendelea na jukumu lake kuu la usikilizaji wa kesi na utoaji maamuzi kwa wakati. Aidha, Mahakama itakamilisha ujenzi wa Mahakama Kuu Tunguu na kuzifanyia matengenezo Mahakama nyingine za Wete, Konde na Mkokotoni.

96. **Mheshimiwa Spika,** ili kuiwezesha programu hii kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 7,926,200,000.00. Kati ya fedha hizo, Mahakama pekee imekadiriwa kutumia shilingi 6,850,500,000.00, zikiwemo shilingi 4,550,500,000.00 za mishahara na stahiki za watumishi, na shilingi 2,300,000,000.00 za matumizi mengineyo. Mahakama ya Kadhi imekadiriwa kutumia shilingi 1,075,700,000.00 ikiwa ni ruzuku ambapo shilingi 827,700,000.00 zitatumika kwa mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 248,000,000.00 zitatumika kwa matumizi mengineyo. Shilingi 789,353,000.00 zinatarajiwa kukusanywa ili kuchangia mapato ya Serikali ***(viambatanisho 2&3).***

G03 – Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali

Programu: Mageuzi ya Utoaji wa Huduma za Sheria na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

97. Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu itaendelea kutekeleza jukumu lake la kuishauri Serikali katika masuala ya kisheria. Katika kipindi hiki, Ofisi itatayarisha miswada ya kisheria, itasimamia na kutoa ushauri wa mikataba, kutayarisha kanuni na matangazo ya kisheria. Uwezo wa watendaji utaimarishwa kwa kuwapatia fursa za mafunzo na vitendea kazi muhimu.

98. Mheshimiwa Spika, ili Ofisi ya Mwanasheria Mkuu iweze kutekeleze majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa Fedha 2020/2021 naliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha shilingi 2,273,100,000.00 kwa matumizi ya kazi za kawaida. Shilingi 903,300,000.00 zitatumika kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,369,800,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 2).***

G04 – Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka

Programu: Uendeshaji na Usimamizi wa Kesi za Jinai na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

99. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2020/2021 Ofisi inatarajia kuendesha kesi 5,000 katika mahakama mbali mbali za Unguja na Pemba. Aidha Ofisi inatarajia

kuwapatia mafunzo ya muda mrefu watumishi wawili na mafunzo ya muda mfupi watumishi 15 ili kuongeza ujuzi, maarifa na ufanisi katika kutekeleza majukumu ya kazi.

100. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka 2020/2021 Ofisi imepanga kuendelea kuimarisha uendeshaji wa mashtaka hasa kwa kesi za udhalilishaji wa kijinsia, madawa ya kulevya na makosa ya uhujumu wa uchumi; kuwajengea uwezo Mawakili wa Serikali ili kuweza kushughulikia kiutaalamu makosa ya jinai yanayoibua changamoto kubwa kwa jamii na Serikali; Kushirikisha wahusika wote wa mfumo jinai wakiwemo wananchi juu ya kuwa tayari kukuza ushirikiano katika kuendesha kesi za jinai kwa haraka; na kuimarisha mazingira ya kutendea kazi ikiwemo upatikanaji wa vitendea kazi.

101. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka kutekeleza majukumu yake kwa mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 3,754,700,000.00. Kati ya Fedha hizo, shilingi 3,154,700,000.00 ni kwa matumizi ya kazi za kawaida zikiwemo shilingi 2,974,800,000.00 (mishahara shilingi 1,703,300,000.00 na matumizi mengineyo shilingi 1,271,500,000.00); shilingi 179,900,000.00 za ruzuku ya uendeshaji Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti na shilingi 600,000,000.00 za maendeleo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti. Kadhalika, Kituo hicho cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti kinatarajia kukusanya shilingi 150,000,000.00 ***(kiambatanisho nam. 2,3&4 vinahusika).***

G05 – Tume ya Kurekebisha Sheria

Programu: Mapitio ya Sheria za Zanzibar na Usimamizi wa Shughuli za Utawala

102. Mheshimiwa Spika, kupitia program hii, Tume ya Kurekebisha Sheria imepanga kuifanyia mapitio sheria ya Mwenendo wa Madai Sura ya 8/1917. Vile vile, Tume itaendelea kutoa elimu kwa umma na kuimarisha utendaji wa kazi kwa kushirikiana na Taasisi zenye majukumu sawa na Tume kitaifa, kikanda na kimataifa.

103. Mheshimiwa Spika, ili kuiwezesha Tume ya Kurekebisha Sheria kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021, naliomba Baraza lako Tukufu kuidhinisha shilingi 1,173,500,000.00. Kati ya fedha hizo shilingi 360,500,000.00 kwa matumizi ya mishahara na stahiki za watumishi na shilingi 813,000,000.00 kwa matumizi mengineyo ***(kiambatanisho nam. 2).***

SHUKURANI

104. Mheshimiwa Spika, baada ya kutoa maelezo hayo, nachukua fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele yenu. Nachukua fursa hii kuwashukuru Washirika wa Maendeleo waliochangia kwa namna moja au nyingine katika utendaji wa vyombo vya Sheria na vyombo vya Dini Zanzibar. Miongoni mwao ni: UNDP, Legal Service Facility (LSF), UNICEF, Direct Aid (Kuwait), Benki ya Maendeleo ya Kiislam

(IDB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Save the Children na Wizara ya Awkaaf ya Algeria. Wizara ya Katiba na Sheria inazishukuru nchi za China, India, Korea, Saudi Arabia, Oman, Uturuki na Misri. Wizara inatoa shukrani kwa Vyombo vya Sheria vya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, nazishukuru taasisi zote za sheria zisizo za kiserikali ikiwemo Jumuiya ya Wanasheria Zanzibar (ZLS), Kituo cha Huduma za Sheria Zanzibar (ZLSC), Jumuiya za Wasaidizi wa Sheria Unguja na Pemba na Chama cha Wanasheria Wanawake (ZAFELA); Jumuiya ya Muzdalifa, Jumuiya na Taasisi mbali mbali za kidini vikiwemo Vikundi vinavyosafirisha mahujaji na taasisi za misaada ya kheri Zanzibar. Sina budi pia kuvishukuru vyombo vya habari kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kutoa elimu na kutangaza matukio mbali mbali yanayohusu shughuli za Wizara ya Katiba na Sheria.

105. Mheshimiwa Spika, kwa ujumla naomba niwashukuru wote waliohusika katika kuifikisha Sekta ya Sheria na upatikanaji wa haki hapa ilipo leo. Ninawashukuru Waheshimiwa Mawaziri na Makatibu Wakuu wote waliowahi kusimamia majukumu ya Sekta ya Sheria kuanzia mwaka 2010. Aidha, ninazishukuru Wizara, Idara na Taasisi ambazo zimefanyakazi pamoja na Sekta ya Sheria. Ninamshukuru Mheshimiwa Jaji Mkuu, Mheshimiwa Mufti wa Zanzibar na Mheshimiwa Mwanasheria Mkuu kwa kufanyakazi nami kwa namna iliyotuwezesha kufikia mafanikio haya tunayojivunia leo. Vile vile, ninamshukuru Mrajis wa Mahakama na Manaibu Warajis wake,

Mtendaji Mkuu wa Mahakama, Waheshimiwa Majaji na Mahakimu wote; Mheshimiwa Kadhi Mkuu, Naibu Kadhi Mkuu na Makadhi wote wa Wilaya; Mheshimiwa Naibu Mwanasheria Mkuu, Wakurugenzi katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; Mwenyekiti wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Katibu na Makamishna wa Tume ya Kurekebisha Sheria, Mkurugenzi wa Mashtaka, Naibu Mkurugenzi wa Mashtaka, na Waendesha Mashtaka wote Unguja na Pemba; Katibu Mtendaji wa Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana; Mwenyekiti na Wajumbe wa Bodi ya Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana; na Katibu wa Mufti wa Zanzibar.

106. Mheshimiwa Spika, kwa namna ya kipekee kabisa ninamshukuru Katibu Mkuu Wizara ya Katiba na Sheria, Ndugu George Kazi, kwa utendaji wake uliotukuka aliouonesha. Kutokana na mchango wake, Wizara ya Katiba na Sheria imeweka misingi muhimu ya utendaji kazi. Ninamtakia mafanikio zaidi katika utendaji wake katika kipindi kijacho. Aidha, ninamshukuru Mshauri wangu katika Masuala ya Kidini, Sheikh Fadhil Suleiman Soraga. Amenisaidia sana kushughulikia masuala mazito yaliyohusu dini na mahusiano ya taasisi za kidini. Ninawashukuru Wakurugenzi na Watumishi wote wa Idara na Taasisi za Wizara ya Katiba na Sheria kwa ushirikiano walionipatia katika kipindi chote cha uongozi wangu katika Wizara hii na ninawatakia kheri nyingi. Aidha, ninawaasa kuwa waendelee kulitumikia taifa letu kwa moyo wote.

HITIMISHO

107. Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie kwa kuendelea kumwomba Mwenyeezi Mungu Mtukufu atuondoshee janga hili la maradhi ya korona na aturejeshe katika hali ya amani. Aidha, ninaiombea nchi yetu iende salama katika harakati za Uchaguzi Mkuu na Mwenyeezi Mungu atujaalie kupata viongozi bora watakaoendeleza mafanikio makubwa ya kupigiwa mfano yaliyopatikana katika awamu nyingine zilizotangulia na kuimarishwa katika Awamu ya Saba chini ya kiongozi wetu mahiri Dkt. Ali Mohamed Shein. Nimalizie kwa kumtakia afya njema kiongozi wetu huyu katika kipindi chake cha mapumziko baada ya kuiongoza nchi yetu kwa kipindi cha miaka kumi, amin.

108. Mheshimiwa Spika, naomba Wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimaye waiidhinishie Wizara ya Katiba na Sheria shilingi 23,204,200,000.00 kutekeleza kazi za kawaida na za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Kati ya fedha hizo, shilingi 19,550,200,000.00 ni kwa matumizi ya kawaida ambapo mishahara ni shilingi 10,269,400,000.00 na matumizi mengineyo ni shilingi 9,280,800,000.00. Shilingi 3,654,000,000.00 ni kwa matumizi ya maendeleo zikiwemo shilingi 2,100,000,000.00 kutoka Serikalini na shilingi 1,554,000,000.00 zinatoka UNDP. Aidha, zipo fedha za ruzuku shilingi 3,004,700,000.00 zinazojumuisha shilingi 1,443,500,000.00 za mishahara na shilingi

1,561,200,000.00 za matumizi mengineyo. Fedha hizi zimeelekezwa katika Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana, Skuli ya Sheria, Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti na Mahakama ya Kadhi ***(Viambatanisho 2&4 vinahusika).***

109. Mheshimiwa Spika, naomba pia Baraza lako liikubalie Wizara ya Katiba na Sheria ichangie shilingi 845,053,000.00 kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali. ***(Kiambatanisho nam. 3).***

110. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

Kiambatanisho 1: Muhtasari wa Upatikanaji wa Fedha, 2019/20

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
Mipango Sera na Utafiti	396,285,000	111,895,000	284,390,000	240,800,240	61	81,530,365	73	159,269,875	56
Uendeshaji na Utumishi	916,819,400	523,126,000	393,693,400	624,492,291	68	400,509,580	77	223,982,711	57
Ofisi Kuu Pemba	401,065,600	238,149,000	162,916,600	230,253,861	57	128,895,935	54	101,357,926	62
Ofisi ya Mufti	800,030,000	377,030,000	423,000,000	538,113,579	67	340,418,002	90	197,695,577	47

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
Mahakama	6,214,400,000	4,411,100,000	1,803,300,000	4,848,064,002	78	3,407,352,355	77	1,440,711,647	80
Ofisi ya Mwanasheria Mkuu	2,114,300,000	736,400,000	1,377,900,000	1,291,268,695	61	593,314,395	81	697,954,300	51
Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka	2,869,500,000	1,669,900,000	1,199,600,000	1,603,694,875	56	1,074,235,250	64	529,459,625	44
Tume ya	1,090,500,000	320,000,000	770,500,000	715,741,137	66	250,763,220	78	464,977,917	60

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
Kurekebisha Sheria									
Ruzuku Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana	1,092,200,000	582,100,000	510,100,000	766,699,724	70	399,931,790	69	366,767,934	72
Ruzuku ya Mahakama ya Kadhi	1,635,500,003	838,686,660	796,813,343	784,595,068	48	616,759,290	74	167,835,778	21
Ruzuku DPP	20,800,000		20,800,000	13,866,664	67			13,866,664	67

FUNGU/IDARA	JUMLA YA MATUMIZI YA KAWAIDA	MISHAHARA NA MAPOSHO	MATUMIZI MENGINEYO	JUMLA YA FEDHA ZILIZOPATIKANA	%	MISHAHARA ILIYOPATIKANA	%	MATUMIZI MENGINEYO ZILIZOPATIKANA	%
JUMLA KUU	**17,551,400,003**	**9,808,386,660**	**7,743,013,343**	**11,657,590,136**	**66**	**7,293,710,182**	**74**	**4,363,879,954**	**56**
JUMLA G10	**2,514,200,000**	**1,250,200,000**	**1,264,000,000**	**1,633,659,971**	**65**	**951,353,882**	**76**	**682,306,089**	**54**
JUMLA G02 - G05	**12,288,700,000**	**7,137,400,000**	**5,151,300,000**	**8,458,768,709**	**69**	**5,325,665,220**	**75**	**3,133,103,489**	**61**
JUMLA YA RUZUKU	**2,748,500,003**	**1,420,786,660**	**1,327,713,343**	**1,565,161,456**	**57**	**1,016,691,080**	**72**	**548,470,376**	**41**
JUMLA G10-G05	**14,802,900,000**	**8,387,600,000**	**6,415,300,000**	**10,092,428,680**	**68**	**6,277,019,102**	**75**	**3,815,409,578**	**59**

Kiambatanisho 2: Muelekeo wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G02- Mahakama	6,850,500,000	4,550,500,000	2,300,000,000				6,850,500,000
G03-Ofisi ya M/Mkuu	2,273,100,000	903,300,000	1,369,800,000				2,273,100,000
G04-Ofisi ya M/Mashtaka	2,974,800,000	1,703,300,000	1,271,500,000	600,000,000		600,000,000	3,574,800,000
G05-Tume ya K/Sheria	1,173,500,000	360,500,000	813,000,000				1,173,500,000
G10-Idara ya	1,250,327,220	476,633,820	773,693,400				1,250,327,220

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
Uendeshaji na Utumishi							
G10-Ofisi Kuu Pemba	485,922,120	183,005,520	302,916,600				485,922,120
G10-Idara ya Mipango, Sera na Utafiti	324,079,320	110,189,820	213,889,500	1,500,000,000	1,554,000,000	3,054,000,000	3,378,079,320
G10-Ofisi ya Mufti	932,682,320	429,682,320	503,000,000				932,682,320
G10- Idara ya	280,589,020	108,788,520	171,800,500				280,589,020

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
Msaada wa Kisheria							
G10-Ruzuku KWNMA	1,229,100,000	545,800,000	683,300,000				1,229,100,000
G10-Ruzuku Skuli ya Sheria	520,000,000	70,000,000	450,000,000				520,000,000
G02-Ruzuku Mahakama ya Kadhi	1,075,700,000	827,700,000	248,000,000				1,075,700,000

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
G04-Ruzuku Ofisi ya M/Mashtaka	179,900,000		179,900,000				179,900,000
Jumla ya Ruzuku G10	1,749,100,000	615,800,000	1,133,300,000				1,749,100,000
Jumla DPP + Ruzuku	3,154,700,000	1,703,300,000	1,451,400,000	600,000,000		600,000,000	3,754,700,000
Jumla Mahakama + Ruzuku	7,926,200,000	5,378,200,000	2,548,000,000				7,926,200,000

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
Jumla ya Ruzuku G02-05	1,255,600,000	827,700,000	427,900,000				1,255,600,000
Jumla ya Rzk	3,004,700,000	1,443,500,000	1,561,200,000				3,004,700,000
Vote G10	**3,273,600,000**	**1,308,300,000**	**1,965,300,000**	**1,500,000,000**	**1,554,000,000**	**3,054,000,000**	**6,327,600,000**
Jumla G10& Ruzuku G10	**5,022,700,000**	**1,924,100,000**	**3,098,600,000**	**1,500,000,000**	**1,554,000,000**	**3,054,000,000**	**8,076,700,000**
Vote G02- G05	**13,271,900,000**	**7,517,600,000**	**5,754,300,000**	**600,000,000**		**600,000,000**	**13,871,900,000**
Jumla G10 - G5	**16,545,500,000**	**8,825,900,000**	**7,719,600,000**	**2,100,000,000**	**1,554,000,000**	**3,654,000,000**	**20,199,500,000**

FUNGU /IDARA	KAZI ZA KAWAIDA				KAZI ZA MAENDELEO		
	JUMLA	MISHAHARA NA STAHIKI	MATUMIZI MENGINEYO	SMZ	WAHISANI	JUMLA MAENDELEO	JUMLA KUU
Jumla Kuu	19,550,200,000	10,269,400,000	9,280,800,000	2,100,000,000	1,554,000,000	3,654,000,000	23,204,200,000

Kiambatanisho 3: Makusanyo ya Mapato kwa Julai-Machi 2019/2020 na Makadirio ya 2020/2021

Kifungu	Idara /Taasisi	Makadirio 2019/2020	Makusanyo Halisi	%	Makadirio 2020/2021
G10	**G10 Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana**	82,190,000.00	52,608,374.00	64	55,700,000.00
G02	**G02 Mahakama**	710,310,000.00	417,621,262.00	59	789,353,000.00
G04	**G04 Kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti**	90,000,000.00	80,000,000.00	89	150,000,000.00
	Jumla	882,500,000.00	550,229,636.00	62	995,053,000.00
	Zinazoingizwa Mfuko Mkuu wa Serikali	**792,500,000,00**	**470,229,636.00**	**59**	**845,053,000.00**

Kiambatanisho 4: Miradi ya Maendeleo 2020/2021

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Washirika wa Maendeleo	Maelezo/Jumla
	Ujenzi wa Jengo la Mahakama Kuu Tunguu			Fedha za Mradi huu zimewekwa Wizara ya Fedha na Mipango
	Ujenzi wa kituo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti	600,000,000		
00000P006	Mradi wa Kuimarisha Uwezeshaji na Upatikanaji wa Haki (LEAP)	1,500,000,000	1,554,000,000	Mradi huu unafadhiliwa na UNDP

Namba ya Mradi	Jina la Mradi	Mchango wa Serikali	Washirika wa Maendeleo	Maelezo/Jumla
	Jumla Kuu	**2,100,000,000**	**1,554,000,000**	**3,654,000,000**

Kiambatanisho 5a: Muundo wa Wizara ya Katiba na Sheria

Wizara ya Katiba na Sheria inaundwa na Idara na Taasisi zifuatazo: -

i. Idara ya Uendeshaji na Utumishi
ii. Idara ya Mipango, Sera na Utafiti
iii. Ofisi Kuu Pemba
iv. Idara ya Msaada wa Kisheria
v. Skuli ya Sheria
vi. Ofisi ya Mufti na
vii. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana

Wizara pia inasimamia Taasisi za Sheria zinazojitegemea ambazo ni: -

viii. Mahakama Kuu
ix. Ofisi ya Mwanasheria Mkuu
x. Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka
xi. Tume ya Kurekebisha Sheria

Taasisi za Wizara ambazo zinapokea Ruzuku ni: -

i. Chuo cha Mafunzo ya Sheria na Utafiti (G04)
ii. Mahakama ya Kadhi (G02)
iii. Skuli ya Sheria (G10)
iv. Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana (G10)

Kiambatanisho 5b: G10 – Programu Kuu, Programu Ndogo na Huduma

Programu	Programu Ndogo	Huduma
1. Programu ya Usimamizi wa Katiba na Sheria	1.Programu Ndogo ya Usimamizi wa Utoaji Huduma za Kisheria	1. Kuratibu Masuala ya Kisheria 2.Kuratibu na Kutoa Msaada wa Kisheria 3Kutoa elimu ya Sheria
2. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Dini	1.Programu Ndogo ya Usimamizi na Uratibu wa Taasisi na Masuala ya Kiislamu	1. Kuratibu na Kusimamia Misikiti, Madrassa, Taasisi na Masuala ya Kidini
		2.Usimamizi wa Mirathi, Wakfu, Amana, Zakka na Shughuli za Kiislamu

Programu	Programu Ndogo	Huduma
3. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara ya Katiba na Sheria	1.Programu Ndogo ya Utawala na Uendeshaji	1. Uendeshaji na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Katika Wizara
	2.Uratibu wa Mipango, Sera na Tafiti	2. Uratibu wa Shughuli za Mipango, Sera na Utafiti 3.Uratibu wa Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo
	1. Uratibu wa Wizara Pemba	4.Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba

Kiambatanisho 6a: Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2019/2020

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mahakama ya Rufaa Tanzania	16					13	12	3	3
M/Kuu Vuga	122	46	1	12	2	44		20	1
M/Kuu Pemba	53	2		3		23	2	25	1
Mahakama ya kazi	31	31							
Mahakama ya Biashara	6	6							
M/Kadhi Rufaa Z	45					45	9		
M/ Kadhi Rufaa P	8					8	5		
M/ Mkoa Vuga	344	10	1	329	32	4		1	
M/Mkoa	154	5		143	24	1		5	3

Kiambatanisho 6a: Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2019/2020

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Mfenesini									
Mkoa Mwera	134	2		131	28	1			
Mkoa Wete	98	2	1	96	67				
Mkoa Chake Chake	149			145	42			4	
Wilaya Mw/kwe	680	32	7	638	503	10	4		
Wilaya Mwera	67	2	0	65	25				
Wilaya Mkokotoni	191	133	119	57	49	1	1		
Wilaya Mfenesini	101	2		99	55				
Wilaya Makunduchi	46	4	1	42	23				
Wilaya Mkoani	147	3		142	119	1		1	

Kiambatanisho 6a: Ufunguaji wa Kesi Mahakamani 2019/2020

	KESI ZILIZOFUNGULIWA					RUFAA			
		Madai		Jinai		Madai		Jinai	
Mahakama	**Jumla Zilizofunguliwa**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**	**Zilizofunguliwa**	**Zilizotolewa Uamuzi**
Wilaya Chake Chake	127			125	26	1		1	1
Wilaya Wete	49	2	2	46	30	1			
Wilaya Konde	37			37	30				
Watoto Vuga	97	67	19	30	4				
Watoto Chake	26	2	1	24					
Watoto Wete	3			3					
M/Watoto Mahonda	18	6		12					
Jumla	**2,749**	**357**	**152**	**2,179**	**1,059**	**153**	**33**	**60**	**9**

Kiambatanisho 6b: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Mwanzo 2019/2020

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Mwanzo					
		Kesi za Madai		Kesi za Jinai	
Mahakama ya Mwanzo	**Jumla**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizoamuliwa**	**Zilizo funguliwa**	**Zilizoamuliwa**
Manispaa Malindi	733			733	689
Manispaa Chake Chake	50			50	42
M/kwerekwe	979	149	33	830	777
Mwera	131	15	11	116	108
Mfenesini	267	8	5	259	251
Mkokotoni	242	18	9	224	212
Makunduchi	59	5	3	54	54
Chwaka	24	1		23	13
Mkoani	68	7	4	61	57
Kengeja	28	4	2	24	11
Chake Chake	292	7	2	285	226
Wete	164	2		162	154
Konde	91	4		87	84
Jumla	**3,128**	**220**	**69**	**2,908**	**2,676**

Kiambatanisho 6c: Ufunguaji wa Kesi katika Mahakama za Kadhi 2019/2020

Ufunguaji wa Kesi Mahakama za Kadhi		
Mahakama za Kadhi Wilaya	**Kesi za Madai**	
	Zilizofunguliwa	**Zilizotolewa uamuzi**
M/Kwekwe	736	410
Mwera	56	22
Mfenesini	99	71
Mkokotoni	131	113
Makunduchi	25	12
Chwaka	5	2
Mkoani	64	27
Kengeja	13	8
Chake Chake	159	102
Wete	76	41
Konde	48	28
Jumla	**1,412**	**836**

Kiambatanisho 7a: Miswada ya Sheria 2019/20

Miswada
1. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbali mbali na kuweka masharti bora ndani yake
2. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Barabara Zanzibar
3. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Wakala wa Serikali Mtandao pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo
4. Mswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Kuanzisha Ofisi ya Mufti Nam.9 ya 2001
5. Mswada wa Sheria ya Kuweka Masharti yanayohusiana na Haki na Huduma za Ustawi wa Wazee na Kuanzisha Mpango wa Pensheni ya Jamii, Usimamizi wake na mambo mengine yanayohusiana na hayo
6. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mawakili Sura ya 28 na Sheria ya Wakuu wa Viapo Sura ya 29 na Kutunga Sheria ya Mawakili na mambo mengine yanayohusiana na hayo
7. Mswada wa Marekebisho ya Sheria ya Usalama Barabarani Sheria Nam.7 ya mwaka 2003.
8. Mswada wa Sheria ya Kuanzisha Skuli ya Sheria Zanzibar
9. Mswada wa Sheria ya Kufuta na Kuanzisha Wakala wa Sheria ya Viwango Zanzibar mwaka 2020
10. Msawada wa Sheria ya Kuanzisha Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Mifugo Zanzibar.
11. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Nam. 8 ya mwaka 2012

na Kuanzisha upya Sheria ya Utafiti wa Kilimo Zanzibar mwaka 2020.
12. Mswada wa Sheria ya Usajili na Usimamizi wa Wataalamu wa Maabara, Tiba na mambo mengine yanayohusiana na hayo
13. Msawada wa Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Afya
14. Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Vileo Sura ya 163 ya 1928 na Kuanzisha Sheria ya Udhibiti, Usimamizi, Usambazaji na Utumiaji wa Vileo na mambo mengine yanayohusiana na hayo.
15. Msawada wa Sheria ya Diaspora ya Zanzibar ya 2020
16. Msawada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Mambo ya Rais 1993 na Kutunga Sheria mpya

Kiambatanisho 7b: Matangazo ya Kisheria - Ofisi ya Mwanasheria Mkuu 2019/20

Matangazo ya Kisheria
1. Proclamation.
2. The tax Administration and Procedure.
3. Presidential Pardon.
4. Prescription of Additional Area of Consideration.
5. Declaration of Adjudication Section.
6. Appointment of Receiving Officers, Sampling Officers and DNA Analysts
7. Appointment of the Chairperson of the Advisory Body of Mnazimoja Hospital
8. Uteuzi wa Maafisa Kazi.
9. Road Closure and Restriction of Traffic and One-way Traffic.
10. List of Fees for Registration of Land.
11. Appointment of The Managing Director of the PBZ.
12. Appointment of Deputy Principal Secretary in the Ministry of Finance and Planning Zanzibar.
13. Appointment of the Commissioner of Budget in the Ministry of Finance and

Matangazo ya Kisheria
Planning Zanzibar.
14. Appointment of Deputy Accountant General in the Ministry of Finance and Planning Zanzibar
15. Appointment of Directors.
16. Kanuni za Kuweka utaratibu wa Utoaji wa Huduma zinazotolewa na Wakala wa Serikali wa Uchapaji.
17. Appointment of the Members of the Board Directors of the Zanzibar Ports Cooperation.
18. Appointment of the Director General of the Bureau of Standards
19. Appointment of the Chairperson of the Board of Zanzibar State Trading Cooperation.
20. Appointment of the Values Officer
21. Appointment of the Chairmen of Zanzibar Swahili Council.
22. Kanuni za Hijja
23. Appointment of the Executive Director of Zanzibar Civil Status Registration
24. Appointment of the Commissioner.
25. The Field Storage Tank Regulations, 2019.

Matangazo ya Kisheria
26. The Packaging of Goods Regulations 2019.
27. The Sales of Liquefied Petroleum Gas Regulation 2019
28. The Metrological Control of Water Meters Regulation, 2019.
29. The Sand and other Ballast Regulation, 2019.
30. The Urban Municipal Council Solid Waste Management Regulations, 2019.
31. DNA Service Regulations, 2019.
32. Kanuni za Msaada wa Kisheria 2019
33. The Zanzibar Development Fund for the Person with Disabilities Regulations, 2019.
34. The Standards for Architectural Design and Construction Regulations, 2019.
35. The Petroleum (Making and Qualify Control) Regulations, 2019.
36. Fees and Levies (Amendment) Regulations.
37. The Petroleum Filling Stations Regulations, 2019.
38. Amendment of the Schedule.
39. The Copyright (Procedures for Rent or Reproduction of Copyright Works) Regulations
40. Regulations for Registration of member and their Works.

Matangazo ya Kisheria
41. Environmental Assessment Regulations, 2019.
42. Appointment of the Chief of Valantia.
43. The Disposal of unfit and Condemned Products Regulations, 2019.
44. Uteuzi wa Waendesha Mashtaka

Kiambatanisho 8a: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji 2019 – UTAHIZA

Taasisi	Maombi	Halisi
1. Ahlusunna waljamaa Hajj & Umra Trust	100	77
2. Albir Hajj, Umra & travelling Agency	60	50
3. Al firdaus Hajj Group	65	65
4. Alnoor Hajj & Travelling Agency	60	60
5. Alsafaa Hajj & Umra Trust	50	60
6. Alharamain Development Foundation	100	100
7. Alhuda Hajj, Umra & Travelling Limited	50	50
8. Aljazeera Hajj & Umra Travelling Agency	130	146
9. Hajj Assistance Group	51	24
10. Haj Caravan Group	65	65
11. Ikram Hajj & Umra Trust	124	124
12. Labayka Hajj, Umra and Trav. Agency	50	40
13. Tahfidh Hajj Group	50	50

Taasisi	Maombi	Halisi
14. Talbiya Hajj, Umra and Travelling Agency	50	50
15. Taufiq Hajj and Travelling Agency	50	60
16. Tawheed Development Network	110	100
17. Tatwawwue Hajj & Travelling Agency	70	50
18. Zanzibar Daawat Wal-Irshad Association	60	60
19. Zanzibar Imams Association	90	117
20. Zanzibar Hajj & Travelling Agency	100	105
21. Zanzibar Istiqama Hajj & Trav. Agency	135	127
22. Zanzibar Istiqama Charitable Organisat.	100	90
Jumla	**1,720**	**1,670**

Kiambatanisho 8b: Taasisi Zilizosafirisha Mahujaji - BAKWATA

Taasisi	Maombi	Halisi
1. Ahlu Daawa Hajj & Travelling Agency	180	180
2. Albushra Tours	70	70
3. Al Husnaa Hajj Trust	55	55
4. BAKWATA	100	100
5. Dalai	60	-
6. Hajj Trust	100	100
7. Ibnu Tayma	55	-
8. Jamarat	50	50
9. Khibar	117	16
10. Labaika Travel	100	120
11. Masjid Adil	100	80
12. Mz Travel	55	60
13. Peace Travel	80	60
14. TCDO	63	-
15. Zamzam	100	95

Taasisi	Maombi	Halisi
Jumla	**1,250**	**981**